

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA KUMI NA SITA NA KUMI NA SABA**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA TANO**

**(DAILY SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS)**

**10 NOVEMBA, 2014**

## **MKUTANO WA KUMI NA SITA NA KUMI NA SABA**

**KIKAO CHA TANO – TAREHE 10 NOVEMBA, 2014**

### **I. DUA**

Mhe. Job Y. Ndugai (Naibu Spika) Alisoma Dua na kuliongoza Bunge.

#### **Waliokuwepo Mezani ni:-**

1. Ndg. Lawrence Makigi
2. Ndg. Neema Msangi
3. Ndg. Zainabu Issa

### **II. MASWALI**

Maswali yafuatayo yaliulizwa na waheshimiwa Wabunge:-

#### **1) OFISI YA WAZIRI MKUU**

Swali Na. 52 – Mhe. Moses Machali Kny. Mhe. Dkt. Festus Bulugu Limbu

#### **NYONGEZA:-**

- (i) Mhe. Moses Machali

Swali Na. 53 – Mhe. Rachel Robert Mashishanga

#### **NYONGEZA:-**

- (i) Mhe. Rechel Mashishanga Robert
- (ii) Mhe. Ester Amos Bulaya

**2) WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**

Swali Na. 54 Mhe. Joseph Roman Selasini ( k.n.y MHE. JOSHUA S. NASSARI)

NYONGEZA

- (i) Mhe. Roman Selasin

Swali Na. 55 – Mhe. Kuruthum Jumanne Mchuchuli

NYONGEZA:-

- (i) Mhe. Kuruthum Mchuchuli
- (ii) Mhe. Masaid Abdalla Seleman

**3) WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Swali Na. 56 – Mhe. Waride Bakar Jabu

NYONGEZA:-

- (i) Mhe. Ester Amos Bulaya
- (ii) Mhe. Selemani Said Jafo

Swali Na. 57 – Mhe. Moshi Selemani Kakoso

NYONGEZA

- (i) Mhe. Moshi Selemani Kakoso
- (ii) Mhe. Said Amour Arfi

**4) WIZARA YA UCHUKUZI**

Swali Na. 58 – Mhe. Maryam Salum Msabaha

NYONGEZA:-

- (i) Mhe. Maryam Salum Msabaha
- (ii) Mhe. Leticia Mageni Nyerere

Swali Na. 59 – Mhe. Augustino Mnanyanda Masеле

NYONGEZA

- (ii) Mhe. Austino Manyanda Masèle
- (iii) Mhe. Ally Mohammed Keissy

## 5) WIZARA YA FEDHA

Swali Na. 60 – Mhe. Fakharia Shomar Khamis

NYONGEZA

- (i) Mhe. Fakharia Shomar Khamis
- (ii) Mhe. Sabreena Sungura
- (iii) Mhe. Mohamed Habib Mnyaa

Swali Na. 61 – Mhe. Mendrad Lutengano Kigola

NYONGEZA:-

- (i) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola
- (ii) Mhe. Salum Khalfan Barwany

Swali Na. 62 – Mhe. Kombo Khamisi Kombo

NYONGEZA

- (i) Mhe. Kombo Khamisi Kombo

## 6) WIZARA YA NISHATI NA MADINI

Swali Na. 63 – Mhe. Rashid Ali Abdallah

NYONGEZA:-

- (i) Mhe. Rashid Ali Abdallah
- (ii) Mhe. Juma Abdallah Njwayo
- (iii) Mhe. Vita Rashid Kawawa

Swali Na. 64 – Mhe. Gaudence Cassian Kayombo

NYONGEZA

- (i) Mhe. Gaudence Kayombo
- (ii) Mhe. Ally Keissy Mohamed
- (iii) Mhe. Mtutura Abdallah Mtutura

**7) WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

Swali Na. 65 – Mhe. Mch. Israel Natse Kny. Mhe. Cecilia Daniel Pareso

NYONGEZEZA

- (i) Mhe. Cecilia Daniel Paresso
- (ii) Mhe. Zabein Muhaji Mhita

Swali Na. 66 – Mhe. Modestus Dickson Kilufi

NYONGEZA

- (i) Mhe. Modestus Dickson Kiluji

**III. MATANGAZO**

- a) Wageni waliokuja kwaajili ya kulitembelea Bunge na mafunzo walitambuliwa na Bunge;
- b) Vikao vya Kamati mbalimbali za Bunge vilitangazwa;
- c) Mwenyekiti wa Bunge Sports Club – Mhe. Idd Mohammed Azzan aliwatangazia Wabunge kuwa kutakuwa na mashindano ya mpira wa miguu, mpira wa pete, riadha, kuvuta kamba na volleyball.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

1) Mhe. Cecilia Pparesso alisimama kwa kifungu cha 68 (7) kwamba alipouliza swali Na. 65 kuhusiana na matatizo ya wananchi ya Karatu, hakupatiwa majibu sahihi na kuambiwa asisubiri kuleta swali Bungeni, aweze hata kwenda Ofisini Wizarani na akasaidiwa. Je, sio haki Mbunge kuleta swali Bungeni na kuuliza, alitaka mwogozo.

NAIBU SPIKA alimjibu kwamba kwa maoni yake Waziri alikuwa anataka kuboresha mahusiano kwa karibu zaidi na Wabunge kuliko kutegemea maswali yao kuja Bungeni.

2) Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa alisimama katika kifungu cha 68 (7) kuhusu Hoja ya Wabunge kupata ripoti ya IPTL kwamba Waziri William Lukvi ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uratibu wa Bunge) alilihakikishia Bunge kuwa ripoti itawasilishwaBungeni lakini haionekani katika Ratiba.

NAIBU SPIKA alijibu kuwa katika Ratiba inaonesha tarehe 27/11/2014 itawasilishwa ripoti ya PAC, kilichoondolewa ni ripoti ya CAG kwakuwa majibu yaliyokuja hayakuwambatishwa. Hivyo itakakuwa tayari imefanyiwa marekebisho hayo yaani kujumuisha majibu hayo kwenye ripoti ya PAC, itawasilishwa Bungeni.

3) Mhe. Ally Keissy Mohamed aliombba mwongozo kwamba swali la 53 halikujibiwa vizuri kuhusu Deni la MSD litalipwa lini?

4) Mhe. Ester Bulaya aliomba mwongozo kwamba katika Bunge lililopita alitoa maelezo Bunge kuhusu. Cancer ya shingo ya kizazi kwamba kuna tatizo la mashine na kuomba commitment ya Serikali kuokoa maisha ya wagonjwa hao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Raisi, - Mhe Prof. Mark y Mwandosya alisema Serikali itatoa Tamko rasmi kuhusu hali ya tiba, vifaa, uwezo wa madaktari na mipango iliyoko, katika kipindi hiki cha Bunge.

- 5) Mhe. Mussa Haji Kombo alitumia katika kifungu cha 68 (7) kuomba maelezo ya hali ilivyo sasa juu ya taarifa iliyotoka Mahakamani kwamba watuhumiwa wamekuwa wakiadhibiwa kwa kupigwa hata kwa risasi.

NAIBU SPIKA alijibu kwamba swala hili bado liko Mahakamani hivyo litashughulikiwa baadaye.

- 6) Mhe. David Ernest Silinde aliomba mwongozo kuhusu hali ya Wakulima ambao mahindi yao yalinunuliwa na serikali kwa mkopo na **shahiki** ya kulipwa baada ya wiki mbili lakini mpaka leo hawajalipwa. Aliomba serikali itoe kauli kuhusu hali hiyo.

Serikali iliahidi kutoa tamko rasmi kuhusu suala hilo ndani ya wiki hii.

- 7) Mhe. Eng. Mohammed Habib Mnyaa Alisimama kifungu cha 68 (7) kuhusu jambo lililotkea punde Bungeni katika maswali na majibu ambapo Waziri wa Fedha alikiri kuwa Tanzania Bara hakuna chombo cha mapato ya Muungano kama Zanzibar kuna chombo kimoja si jambo ambalo ni kinyume na katiba. Aliomba tamko la Serikali kuhusu hatua zitakazochukuliwa na Serikali kulipa fedha kwa gharama iuliyopotea.

Waziri wa Fedha (Mhe. Saada Mkuya) alijibu kwamba Bara chombo kipo kimoja tu na Serikali iko katika hatua za mwisho katika kuunda mfuko wa pamoja wa fedha ambapo mapato yote ytaatangazwa.

- 8) Mhe. Rukia Kassim Ahmed alisimamia kifungu cha 47 (1) (2) (3) kuhusu serikali kudaiwa na MSD na aliomba kutoa hoja Bunge lisitishwe shughuli zake kujadili suala hilo muhimu linalohusu maisha ya wananchi.

NAIBU SPIKA alijibu kwamba ni kweli hoja hiyo ni muhimu lakini kwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Raisi alisema Serikali itatoa tamko kuhusu suala hilo, basi aliiomba Serikali ifanye haraka kuleta tamko hilo na Bunge lisiporidhika, utaratibu mwingine utafuatwa.

- 9) Mhe. Ally Mohammed Keissy alisimama kusema siyo vibaya kutibiwa nje maana hata wabunge wa CUF pia wapo walioenda kutibiwa nje.
- 10) Mhe. Rashid Ali Abdalla alisimama kwa kifungu cha 68(7) kuomba mwongogo kwamba wakati Naibu Waziri wa Nishati akajibu swali Na. 63 alisema mradi wa kinyerezi II na I haiko kwenye Bajeti ya Serikali.

WAZIRI WA NISHATI MADINI alijibu kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya Bajeti ya Serikali haziwezi kutosha kabisa kusaidia miradi ya nishati.

- 11) Mhe. Rajabu Mbarouk Mohammed alisema katiba kifungu cha 68 (i) na 94 (3) kwamba Kanuni za Bunge kuhusu kuwasilisha mpango wa maendeleo Bungeni umekiukwa kwani siku ya kuwasilisha Mpango ndiyo sahii ilipoanza kujadiliwa kitu ambacho kinasababisha Wabunge kushauriwa kuchangia vizuri mpango huu.

Mhe. Stephen Wasira alijibu kwamba ni kweli vitabu vilichelewa kwa kuwa Kamati ilichelewa kuvileta. Hivyo kuhamisha mjadala kwa sababu hiyo ni kuwanyima haki wananchi.

- 12) Mhe. Moses Machali alisimama katika kifungu cha 68 (7) kwamba wakati Waziri wa Maliasili akijibu swali Na. 65 alilieleza Bunge kwamba hakuna matatizo makubwa sana katika maeneo ya Hifadhi kitu ambacho sio kweli na katibu wa Bunge ametoa barua kwamba Bunge haliwezi kuingilia utekelezaji wa Serikali. Aliomba kujua kuhusu kanuni ya 63 ya Bunge kuisimamia Serikali.

NAIBU SPIKA alijibu kwamba Mhe. Machali awasiliane na Ofisi yake waone jinsi ya kuwasiliana na Serikali.

#### **IV. TAARIFA**

Naibu Spika alilitambulisha Bunge kuhusu Mhe. Samwel Sitta kukaimu nafasi ya kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni.

#### **V. KAMATI YA MIPANGO**

Hoja za Serikali kwamba, Bunge likae kama Kamati ya Mipango ili kujadili na kuishauri Serikali juu ya Mapendekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa kwa mwaka 2015/2016 (Majadiliano yanaendelea)

Waheshimiwa Wabunge walichangia mpango wa maendeleo kama ifuayavyo:-

50. Mhe. Yussufu Salim Hussein
51. Mhe. Dkt. Goodluck – Ole – Medeye
52. Mhe. Said Amour Arfi
53. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi
54. Mhe. Lucy Fidelis Owenya
55. Mhe. Betty Eliezer Machangu
56. Mhe. Joseph Roman Selesini
57. Mhe. Khatib Said Hji
58. Mhe. Moze Abeidy Said

## **VII. KUSITISHA BUNGE**

Saa 7:00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 Jioni

## **VIII. BUNGE KURUDIA**

Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia

## **IX. KAMA YA MIPANGO**

Waheshimiwa Wabunge waliendelea kujadili mapendekkezo ya utekelezaji wa mpango wa Taifa kwa mwaka 2015/2016 kama ifuatavyo:-

10. Mhe. Rashid Ali Abdallah

## **TAARIFA YA SPIKA**

1. Mhe. Charles John Mwijage alitoa Taarifa kwa Msemaji – Mhe. Rashid Ali Abdallah kwamba Rais ana haki ya kutibiwa kama ilivyo kwa Wabunge kutibiwa nje ya nchi.
2. Mhe. Keissy Ally Mohammed alitoa Taarifa kwamba wiki mbili zilizopita kiongozi wa CUF na mkwewe na mtoto wake pia walikwenda India kutibiwa.

Mhe. Mwandosya alijibu taarifa hizo kuwa “Hujafa Hujaumbika.” Yeye ni mmojawapo katika viongozi waendao India na kila akifika huomba list ya wagonjwa kutoka Tanzania na ameona list ni kubwa yenyе majina ya viongozi wengi na watu kwa kawaida wamo ambao hutibiwa nje. Hivyo ni vyema kuwa na staha maana hakuna ajuaye kitampata nini.

NAIBU SPIKA – alisema kabla ya Bunge hili alikwenda India kikazi akapita Apollo Hospital akaona Watanzania wangonjwa kule, hivyo jambo hili liachwe maana siyo vyema kuongelea vibaya wagonjwa.

59. Mhe. Ahmed Juma Ngwali
60. Mhe. Abdul Jabiri Marombwa
61. Mhe. Juma Abdallah Njwajo
62. Mhe. Meshack Jeremiah Opulukwa
63. Mhe. Omar Rashid Nundu
64. Mhe. Said Mussa Zubeir
65. Mhe. Herbet James Mntangi
66. Mhe. Muhammed Ibrahim Sanya
67. Mhe. Eng. Ramo Mataala Makani
68. Mhe. Haroub Mohammed Shamis
69. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga
70. Mhe. John Paul Lwaji
71. Mhe. Mtutura Abdallah Mtutura
72. Mhe. Elizabeth Nkunda Batenge
73. Mhe. Prof. Sospeter Muhongo – Waziri wa Nishati na Madini.

## **XI. KUAHIRISHA BUNGE**

Saa 1.45 usiku Bumge lilahirisha mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 11 Novemba, 2014 saa Tatu Asubuhi.

**DODOMA  
10 NOVEMBA, 2014**

**DKT. T.D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**